# HII NDIO INJILI

*Maisha ni Uhusiano (utangamano)*

## Vipengele muhimu ya Injili Matendo ya - Mitume 8:25-40

**<u>Ufahamu muhimu</u>: maswali mengi kuhusu wokovu yanatokana na utatanishi kuhusu Injili.**

Matendo ya Mitume 8:25-40-inaongea na kue;leza kuhusu towashi wa Kushi. Hadithi hii si ya kawaida kwa sababu hali ya mageuzi inatendeka katika uwezo wa Mungu, mitazomo yote ya Towashi na Filipo inapitia nguvu ya Mungu. Hii ni Picha kamilifu kivyake.

Wazo au dhamiru kuu kwenye vifungu 8, 9, na 10 ni usambazaji na uenezaji wa Injili katika sehemu zote za jamii. Katika kila kifungu, tuna pata hadithi yenye maelezo Fulani kuhusu uenezaji wa Injili. Kifungu cha nane, Yule towashi wa Kushi anabadilisha imani yake na kumwamini Kristo. Kulingana na orodha ya vizazi katika Kitabu cha Mwanzo (Mwanzo 10:6) twapata kwamba kizazi cha Kushi ni wana na uzao wa Hamu. Kifungu cha tisa, twampata Sauli wa Tarso akisimulia hadithi yake. Sauli alikua Muyahudi na wa kizazi cha Shemu (Mwanzo 10:21). Kifungu cha Kumi twapata historia ya kornelio aliyekua Myunani. Kornelio angekua wa uzazi wa Japhethi (Mwanzo 10:2-5).

Hivi vikundi vina wakilisha ethnolojia au mbari za watu Fulani na migawanyiko ya kijiografia baada ya Garika kuu. Hamu, Shemu, na Jafethi wote ni wana wa Nuhu. Mungu alipo ijaza ulimwengu mara ya pili baada ya Garika, kila mmoja akawa wa uzazi wa shemu, Hamu, au Jafethi. Historia hizi hazionyeshi tu kwamba Injili ya badilisha maisha ya watu kadhaa pekee, bali pia Injili yawafikia watu wote katika semu zote tatu za jamii.

Wacha tuangalie historia mojawapo ya zile tatu, na tuangalie vipengele tatu vya kina ya Injili. Kweli za Kanuni hizi ni za watu wote kila mahali ulimwenguni.

### I. INJILI IMETIWA NGUVU NA KAZI ROHO MTAKATIFU WA MUNGU

Ikiwa tuta shindwa kuelewa ukweli huu, ama kuikataa basi hatuna budi kuchnganyikiwa kuhusu wokovu.

Kunazo Kweli tatu Ndani ya Bibilia ambazo zina pinga kwa kina wokovu wa Kibinadamu na kusisi tiza na walimwengu.

- Hakuna anaye okolewa kupitie matengo yake mwenyewe (Waefeso 2:8-9)

Waefeso 2:8-9 yasema, "Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; 9 wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu."
(Vifungu vya kuongezea: Tito 3:5; Wagalatia 2:16)

- Hakuna anayeokolewa kwa sababu ya utakatifu wake (Wafilipi 3:9).

Mtu awaye yote haokolewi kwasababu yeye ni mwema. Kano wanao amini kwamba wataokolewa kwasababu hajawahi tenda jambo baya lolote. Hiyo ni kuto fahamu hali ya dhambi jinsi ilivyo.

Ukiiba peremende kutoka kwa duka, utaitwa mwizi. Haijalishi kama ulichukua mia moja au milioni moja, ama peremende moja. Lile tendo la uizi mara moja lakupa jina Mwizi. Kwa hali hioy hiyo, haijalishi kama ulitenda dhambi mara moja, mara 100, au mara 1,000,000. Kutenda dhambi kwetu kwa tupa Jina Mtenda dhambi.

Warumi 3:23 inanukuu ikisema, "Kwa maana wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu." Si kwa ukubwa wa dhambi zetu au mara ngapi tume tenda dhambi. Ni jinsi dhambi ilivyo na madhara yake kwetu. Dhambi inatutenga mbali na Mungu.
(Vifungu zaidi: Warumi 10:3-4; Wakorintho wa Pili 5:21; Mathayo 6:33; Warumi 4:6)

- Hakuna anayeokolewa na uamuzi wake (Yohana 15:16)

Yohana 15:16, "Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi..." Yohana 6:44, "Hakuna mtu awezaye kuja kwangu, asipovutwa na Baba aliyenipeleka..." Yohana 6:65, Akasema, kwa sababu hiyo nimewaambia ya kwamba hakuna mtu awezaye kuja kwangu isipokuwa amejaliwa na Baba yangu."

Wokovu ni kazi ya Mungu pekee. Chanzo yake ni nguvu na uwezo takatifu wa Mungu (Matendo ya Mitume 13:48; Warumi 8:29; Waefeso 1:3-7) na inafanyika kupitia neema zake (Waefeso 2:8-9; 2 Watheselonika 2:13; 2 Timotheo 2:10; Tito 1:1; 1 Petero 1:1

Mbali na mahojiano haya, kuna vizuizi vikuu dhidi yetu wanadamu kufahamu na kuelewa kwa ndani kibinafsi. Kwanza sisi tumekufa kiroho na hatuwezi kumuitikia Mungu (Waefeso 2:1 inasema, "Nanyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu." Kukufa kimwili inamaanisha mtu hawezi kufanya chochote anavyo paswa kuhisi na kukufa kiroho inamaanisha mtu hawezi kuhisi mambo ya kiroho. Watu waliokufa hawawezi kufanya jambo lolote.

Kizuizi kiku cha pili ni udanganyifu. Paulo aliwaambia wakristo wa Wakorintho, "Lakini kama Injili yetu imesitirika, imesitirika kwa hao wano potea; ambao ndani yao mungu wa dunia hii amepufusha fikira zai wasioamini, isiwazukie nuru ya Injili ya utukufu wake Kristo aliye sura yake Mungu." (2 Wakorintho 4:3-4). Shetani na mapepo wake wako kwenye shughuli ya kuwapotosha na kuwa danganya watu ili wasione mwangaza ya Kweli ya Mungu.

Twahitaji Roho Mtakatifu ili aiwezeshe mioyo iliyo kufa na kuziangazia mioyo zilizo danganywa. Wafu hawatendi chochote; na waliondanganywa hawawezi kuamini.

Bibilia inaonyesha wazi kwamba Mungu ametupa njia ya wokovu. Ni kazi ya Roho Mtakatifu kuarakisha roho zilizokufa, kuziangazia ufahamu roho zilizo danganywa, na kutuleta karibu kwa Baba mwenye mapenzi kwetu.

Katika kadithi ya Towashi wa Kushi, Roho Mtakatifu kwa wazi anaonekan anafanya kazi. Alimwzesha Filipo kumpata wakati uliofaa. Mstari wa 26 insema, "Malaika wa Bwana akasema na Filipo akamwambia, Ondoka ukaende upande wa kusini hata njia ile itelemkayo kutoka Yerusalemu kwanda Gaza; nayo ni Jangwa." Mstari wa 29 yatwambia kwamba, "Roho akamwambia Filipo, sogea karibu na gari hili, ukashikamane nalo." Hali iliyo mwongoza Yule towashi wa Kushi kupokea wokovu ilipangwa na Roho Mtakatifu.

Unaweza jadili hili wazo kwamba Roho Mtakatifu alimpa tu huyu Towashu msukumo na maswali tu. Roho Mtakatifu alimtayrisha Filipo na majibu kamili na Roho ndiye aliye mwita Towashi huyu kupokea wokovu.

Twamwitaji Roho atutangulie, kututayarishia njia, na kutuandalia mioyo ya watu kuja kupoipokea wokovu, na kuyaharakisha mioyo zilizo kufa, kuondoa udanganyifu, kuleta ukweli, na kuwaita watu waje katika uhusiano na Mungu.

Pasipo kuwa na kazi ya Roho wa Mungu katimu uenezaji wa Injili, hapana wokovu.

## II. MSINGI WA INJILI IKO NDANI YA UKWAELI WA NENO LA MUNGU

**Neno** la Mungu ni Muhimu katika Wokovu.

- Warumi 10:17: "BAsi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neon la Kristo."
- Yohana 5:24: "Amin, amin, nawaambia, Yeye alisikiaye neon langu na kumwamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele; wala haingii ukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani."
- Waefeso 1:13: "Nanyi pia katika huyo mmekwisha kulisikia neon la kweli, habari njema za wokovu wenu; tena mmekwisha kumwamini yeye, na kutiwa muhuri na Roho Yule wa ahadi aliye mtakatifu."
- 1 Petero 1:23: "Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika; kwa neon la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele."

Roho Mtakatifu ndiye hutufunulia kazi ya Kristo kupitia Neno la Mungu kwetu.

Katika historia kuhusu towashu, alikuwa akisoma Isaya 53. Kifungu hiki kilikuwa kikiongelea Mwana kondoo wa Mungu, lakini hakuwa akielewa maana yake. Filipo alimuuliza, "Je unaelewa unachokisoma?" nnaye akajibu, "Nawezaje kuelewa, kama hakuna wakunifafanulia?" Akamualika Filipo apande kwenye gari lake na kuketi kando yake. Filipo alianzia pale Yule towashi alipofikia na kuelekeza kwa Maandiko, huku akimfafanulia Yesu ni nani, na kile alicho kifanya kabla ya kufa Msalabani.

Filipo alifanya kile Yesu alichofanya katika kitabu cha Yohana 3, kile Paulo alicho fanya 1 Wakorintho 9, Kile Apollos alichokifanya Matendo ya Mitume 18, na chenye Stefano alichokifanya Matendo ya Mitume 7. Hawa wote walifahamu maandiko vyema na wakawafikia watu popote walipokua.

Kama kile tunacho jua ni utaratibu wa Injili, sisi sote tuta changanyikiwa ikiwa majadiliano haya itatuelekeza kwingine. Kama tutailewa mafundisho kamili ya Injili, tutaweza kuwafikia kila mmoja na mahitaji yake na kujibu maswali yao watakapo tuuliza.

## III. INJILI HUENEZWA KUPITIA USHUHUDA WA WALIO WA MUNGU

Mungu amechagua wanadamu kuwa chombo cha kukamilisha kazi yake tukufu (Matendo ya Mitume 2:4,14; 4:8, 31; 6:3-8; 7:55; 8:17; 10:1-48; 16:25-34). Filipo alikuwa chombo kwenye mikono ya Mungu. Alipoamurishwa kwenda, aliende bila kusita. Alipo alikwa kuingia kwenye gari, aliingia. Alipopewa nafasi ya kushiriki katika neon la Kristo, alihubiri Yesu. Filipo alikuwa tayari.

**Mungu huwatumia watu kueneza habari ya Injili yake.**

- Katika Matendo ya Mitume 1:8 Yesu aliwaambia wafuasi wake kwamba watakuwa mashahidi wake. Filio alikuwa shahidi wake kwa Yule towashi.
- Warumi 10:14-15, Paulo alisema, "Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikieje pasipo mhubiri? 15. Tena wahubirije, wasipopelekwa? Kama ilivyoandikwa, Ni Mzuri kama nini miguu yao wahubirio habari njema!"
- 1 Wakorintho 1:21, Paulo anasema, "Kwa maana katika hekima ya Mungu, dunia isipopata kumjua Mungu kwa hekima yake, Mungu alipenda kuwaokoa waaminio kwa upuzi wa lile neon linalohubiriwa." Mungu huwatumia watu wake kutangaza Injili, na hufurahishwa sana anapowaokoa wanao mwamini.

Katika hekima ya Mungu, amechagua kuwatumia watu kueneza injili kote. Tumepewa jukumu la kushirki ujumbe huu na watu wote ulimwenguni. Tumetunukiwa na Habari Njema ya Mungu, na kuamurishwa kupeleka Injili hii pembe zote ulimwenguni.
Mungu amechagua kushiriki habari yake kuu kupitia wanaomwamini. Ametupa Roho wake Mtakatifu. Ametupa Neno Lake. Kisha, ametuamurisha twende tuakeneze Habari yake Njema ya Injili.

Injili inawezaje kufika mwisho wa dunia? **Roho wa Mungu…Neno la Mungu…Watu wa Mungu.**

## Kanuni za utayarishaji Injili-Mariko 4:1-20

**Twaenda** kuangazia kazi ya Roho katika kutayarisha moyo wa mtu kabla ya kupokea Injili. Moja ya mfano mwafaka Kristo ametupa katika kitabu cha Mariko 4:1-20. Ni mfano wa mchanga aina nne.

Bibilia inapo ongelea wokovu, mfano ya kwanza kutumiwa ni ya ukulima. Katika mfano huu, Yesu anataja mchanga ya aina nne. Kila mchanga ina ashiriya hali ya moyo wa mwanadamu na jinsin invyo pokea injili na ujumbe wa Kristo. Vilevile kila aina ya mchnga inaonyesha kiwango tofauti ya maandalizi au utayarisho wa Roho Mtakatifu, kama vile moyo wa mwanadamu invyo elewa . roho wa Mungu anatuezesha kuungana na Mungu badala ya kujaribu kuwsukuma watu kwa Kristo.

Yesu anasema, *"Sikilizeni, Tazama , mpanzi alitoka kwenda kupanda; ikawa alipokuwa akipanda, mbegu nyingine ilianguka kando ya njia, wakaja ndege wakaila."*

Weka pich hii akilini, huyu mtu akitembea kwa njia, akiwa na mfuka wa mbegu kwenye bega lake, huku akiyatapakaa zile mbegu. Anapo sambaza zile mbegu, kunazo zile ziliianguka kwa njia. Zingine zilianguka kwenye mawe. Kunazo zilizoanguka kwenye kwekwe, na zingine kwenye udongo wenye rotuba mchnga mzuri. Hii ndio picha Yesu anatumia kuelezea hali ya moyo wa mwanadamu na jinsi anavyo pokea ama itikia mbegu ya Injili ya Kristo.

**Udongo gumu: kuna wat wasioelewa injili (ms. 3-4, 15):**

**Udongo (ms. 3-4)** *"Sikilizeni, Tazama , mpanzi alitoka kwenda kupanda; ikawa alipokuwa akipanda, mbegu nyingine ilianguka kando ya njia, wakaja ndege wakaila." (NIV)*

*Maelezo ya Udongo (ms.15) "Hawa ndio walio kando ya njia lipanwapo neon; nao, wakiisha kusikia, mara huja Shetani, akiliondoa lile neon lililopandwa mioyoni mwao."*

Mfano huu unapatikana katilka kitabu cha Mathayo 13 na Luka 8. Katika maelezo ya Matahyo 13 tunapata mafundisho zaidi kuhusu udongo wa kwanza. Mathayo 13:19, anasema, "Kila mtu alisikiapo neon la ufalme asielewe nalo, huja Yule mwovu, akalinyakua lililopndwa moyoni mwake." Hii ndio mbegu zilizo anguka kwa njia. Huyu ni mtu asiye elewa Injili. Kama ni matayarisho, mioyo yao hayaja tayarishwa na Roho Mtakatifu. Mioyo yao ni migumu katika maneno ya Mungu. Naye John MacAthur ana haya ya kumuelezea mtu kama huyu:

Sababu za kumfanya asielewe si kwa sababu ya ukosefu katika Injili lakini ni ya ugumu wa Moyo wake. Huyu ni mtu anaye anafahamika kwa kawaida katika Agano la Kale kama mtu mwenye shingo ngumu. Asiye jishughulisha na maneno ya Mungu, na amejitenga na chochote kinacho husiana na maneno ya kiroho. Neno la Mungu haiwezi penya kwenye moyo wake au akilini mwake. Huku hana nafasi ya kufikiria Kuhusu Maandiko, anayaona kama upumbavu. Ameendelea na kila mara kukataa na kuzuia chochote kinacho husiana na Kiroho, yaani udongo wa moyo wake umepondwa hadi haiwezi penyeka na kupotea hisia zake.

Hata hivyo, ingawaje mtu anaweza poteza hisia zake kupokea na kuitikia Injili leo, haimaanishi tuko na sababu ya kuto panda mbegu ya Injili.

**Twawezaje Iktikia au Kuleta ushawishi kwa udongo wa aina hii?**

- **Pray**
  - o **Tuombe Mungu aivunje ugumu wa moyo wa wanadamu kupitia Neno Lake (Warumi 10:14-17)**
  - o **Tuombe ili Mungu afungue macho kuona ukweli (1 Wakorintho 1:18; Matendo ya Mitume 17: 18-20; 26: 18).**
  - o **Tuombe ili Mungu alete ushawishi ndani ya mioyo yao (Matendo ya Mitume 2:37). Wale watu siku ya pentekoste walichomwa mioyoni mwao walipo kutana ana kwa ana na Injili ya Kristo.**

• **Panda Mbegu**

Sehemu ya ugumu wa moyo wa huyu mtu inatokana na ushuhudiaji wa maisha ya kinafiki ya Wakristo wengi. Ulimwengu unamtafuta mtu aliye badilishwa na nguvu ya Mungu, na anaishi kulingana na nguvu hizo zilizo mbadilisha pale awali. Mungu anapo kupa nafasi, kwa unyenyekevu panda mbegu ya Neno la Mungu maishani mwa wengine.

• **Penda bila Masharti**

Hali ya mtu ya kiroho haina uhusiano yoyote na kama tutampenda au la. Ni lazima tukumbukekwamba watu huwageuki karibu na Injili kwa sababu wameelewa neno; hawaelewi Injili. Mpende huyu mtu.s

**Udongo wenye Mawe: kuna watu wasio fahamu garama ya Kumfuata Kristuo (Ms. 5-6, 16-17):**

Udongo (ms.5-6): *"nyingine ikaanguka penye mwamba, pasipokuwa na udongo mwingi; mara ikaota kwa kuwa na udongo haba; hata jua lilipozuka iliungua, na na kwa kuwa haina mizizi ikanyauka."*

Maelezo ya huu udongo (ms. 16-17): *"Kadhalika na hawa ndio wapandwao penye miamba, ambao kwamba wakiisha kulisikia lile neon, mara hulipokea kwa furaha; ila hawana mizizi ndani yao, bali hudumu muda mchache; kasha ikatokea dhiki au udhia kwa ajili ya lile neon, mara hujikwaa."*

**Hali au Sifa ya Udongo: udongo wa pili** ndio tunanaanzia ama msingi wa mjadala wetu. Huyu mtu aliupokea Neno kwa furaha kuu. Je! Haimaanishi kwamba alimpokea Kristo? Huyu mtu alikua kwa muda mfupi. Wanawezaje kukua kama hawaja zaliwa?

Tunapaswa kuwa makini kuhakikisha kuna ishara za toba kutokana na Neno la Mungu. Bibilia haija sema kwamba kukomaa ndio ishara ya toba; bali inaongelea matunda kama kama ishara sawia ya mtu aliye tubu dhambi zake.

Yohana Mbatizaji aliwakemea viongozi wa dini kwa sababu kutamani ubatizo wa utakatifu bila kuonyesha ishara za toba. *"Basi zaeni matunda yapasayo toba."* (Mathayo 3:8).

Yesu alifundisha kwamba tunaweza tofautisha kati ya watu wema na wabaya kwa kuangalia matunda ya maisha yao. *"Kwa maana hakuna mti mzuri uzaao matunda mabaya, wala mti mbaya uzaao matunda mazuri; kwa kuwa kila mti hutambulikana kwa matunda yake; maana, katika miiba hawachumi tini, wala katika michongoma hawachumi zabibu."* (Luka 6:43-44)

Katika Yohana 15, Yesu anasema kwamba yeye in Mzabibu na sisi ni Matawi. Anaendelea na kusema kwamba kila tawi ndani yake lita zaa matunda. Matunda ndio ishara ya wazi ya kuwa ndani ya Kristo. Kwa hivyo, tunapo jifunza mistari kama hii, lazima tujiulize, Je! Tunaweza kuona Matunda?

Udongo wa pili ulio tajwa ni ule wa mwamba. Maelezo haya si ya ile ya mawe madogomadogo. Mkulima anapo lima shamba lake yeye hukusanya yale mawe na kutoa inje ya shamba lake kabla ya kupanda. Lile jiwe lililotajwa hapa ni Mwamba ambao haukufikiwa wakati wa kulima. Hapa tunaona lazima kuwe na maandalizi kabla ya upanzi wa mbegu. Mbegu zilizo anguka kwa njia (ms. 4)hazikuweza kupenya kwenye ardhi. Mbegu zilizo anguka juu ya mwamba (ms. 5) zilipenya kwa mchanga, lakini juujuu.

Mbegu zilizo penya kwa zile mchnga ya juu, "zili kua kwa haraka…lakini jua ilipochomoza, ziliungua." Mizizi hazikuweza kufikia maji. Udongo haikuwa na uwezo ya kunawirisha uhai mmea.

Huyu mtu ameelezewa zaidi katika mistari ya 16-17. *"Kadhalika na hawa ndio wapandwao penye miamba, ambao kwamba wakiisha kulisikia lile neon, mara hulipokea kwa furaha; ila hawana mizizi ndani yao, bali hudumu muda mchache; kasha ikatokea dhiki au udhia kwa ajili ya lile neon, mara hujikwaa."*

Udongo mgumu iliipa neno upinzani na wala haikutaka kuilewa Injili. Udongo wenye mawe mawe iliipokea injili lakini haikuielewa injili wala umuhimu wake. Huyu ni mtu anaye pokea neno kwa jisia zake tu na kwa furaha bila kuwa na msingi bora ya kuielewa umuhimu wake kwa kina.

Msimulizi mmoja alikuwa na haya ya kusema,"Wakati mwingine wanao pokea Inijili kijuujuu inaletwa na enezaji wa neno bila ufasaha ambao unazuia Baraka za Mungu za wokovu na kuficha umuhimu na dhamana yake kama toba, kujikana, na kugeuka kutokana na hali yazamani ya maisha. Wayu wanapo himizwa kuja mbele, kuinua mikono yao, ama kuweka sahihi yao kwenye kadi, bila kufahamu kwa undani Kazi ya Kristo Yesu, wako hatarini yak wenda mbali na Kristo kuliko vile walivyo kuwa awali. Wao huzuiliwa kupata wokovu wa kweli kwa sababu ya ushuhuda wa uwongo wa imani.

Roho mtakatifu angali anatayarisha udongo huu. Badala ya kungoja hadi awe tayari, yeye hufanya uamuzi kwa kufuata hisia zake bila kuwa na ufahmu kamili na umuhimu wa kumfuata Kristo.

Je, mtu mwenye moyo kama wa jime hufanana aje? Huyu ni mtu mwenye hali ya kuwa na hisia nyingi na uamuzi wake huongozwa na hisia zake. Wao hujiusisha na kazi ya Mungu, (Kuhudhuria kanisa, kushiriki katika mafundisho ya Bibilia, na hata kutumika kanisani, n.k.). Lakini, majaribu yanapo wakumba, hawana uweza wa kumsogelea Kristo, inayo fuatia ni kuanguka na kwanda mbali na Kristo.

**Je twawezaje ifikia udongo w aina hii?**

- **Fuata taratibu kama ya udongo wa kwanza**
- **Ni vyema kutambua tama ya kufuata neno, lakini elezea kwa ndani matarajio ya wokovu**
- **Kuwa na wakati mwafaka wa kujibu maswali yoyote kuhusu wokovu**

**Udongo mwenye Mwiba: kuna watu walio na hamu kuu ya ulimwengu kuliko Mungu (ms. 7,18-19):**

**Huu udongo** (ms. 7): "Ingine ikaanguka kwenye miiba; ile miiba ikamea ikaisonga, isizae matunda."

Maelezo kuhusu udongo huu, (Ms. 18-19): "Na hawa ndio wale wapandwao penye miiba; ni watu walisikiao lile neno, na shughuli za dunia, na udanganyifu wa mali, na tama za mambo mengine zikiingia, hilisonga lile neno, likawa halizai."

Jambo letu la kwanza la kuangaziwa ni kuhusu matunda ama kutokuwa na nazao. Bibilia hainaongelei kukua kama kuonyesha maisha ya Mkristo aliye tubu thambi zake bali-ni matunda. (Maandiko zaidi: Mathayo 3,7,13; Yohana 15; Warumi 7; Wagalatia 5; Waefeso 5, Wakolosai 1).

Jambo la pili la kutiliwa kuangazia ni hali ya kuendelea mbeleya matayarisho ya Undongo. Udongo wa kwanza ulikuwa mgumu isio weza penyeka. Udongo wa pili ulillimwa kwa juu, si kwa ndani kupita sehemu gumu ya udongo. Huu wa tatu umelimwa vizuri tayari kupadwa mbegu. Twajua hii kwa sababu kila klicho pandwa kilimea. Kwekwe pia zinakua. Mbegu ya Neno lina kua. Kwekwe zimekua kiwango ya kuisonga lile Neno lilipokua.

Kwa huyu mtu, Mungu yu mojawapo ya mambo mengi anayo fuatilia maishani. Mambo ya ulimwengu hayaja zimwa na Mungu maishani mwake. Wao humwona Mungu kama jambo linalo ongezea yale mengi walio nayo maishani na wala yeye si Maisha yao. Kwa maana wanapo lazika kuchagua kati ya Mungu na Ulimwengu, ulimwengu hushinda kwani

la pewa nafasi ya kwanza. Huyu ni mtu anaye kumbwa na mambo ya maisha (kama vile kazi yake, rehani, kulea familia yake, hali ya uchumi na kutafuta fedha, magari, n.k.), ambazo zinawafanya wakose nafasi ya kutafuta neno la Mungu lenye uzima wa milele. Neno la Mungu husongwa na kukosa kunawiri.

Mara nyingi huyu ni mtu mwenye umri wa makamu. Mototo hashughuliki na mambo wala hana wasisi na vitu vya maisha, starehe ya mali, na tamaa ya vitu vya ulimengu. Maelezo haya ni ya mtu aneye jua ukweli wa Neno la Mungu, lakini wamechagua kufuata vitu vingine na kumuacha Kristo.

Huyu ni mtu vuguvugu ndani ya Mungu lakini ametilia maanani mambo ya ulimwengu. Yeye ni mtu wa kiroho lakini aliyepotea. Ni mtu wa dini asiyekua na uhusiani wa karibu. Hawaja kosa kwanda kanisani, wao wanahusika kanisani, wamemkiri Kristo lakini wamekosa matunda ya kiroho inayo tokana na neno la Mungu.

Matunda ya Mungu hayaonekani maishani Mwao. Hawana furaha maishani mwao. Hakuna amani wakati wa ugumu maishani. Hawana subira na watu wengine. Si watu wenye upole wala unyenyekevu katika kazini mwao. Hawana bidii ya kutafuta utakatifu wa Mungu. Hawana chochote cha kuonyesha maisha yenye matunda ya Roho Mtakatifu.

**Twawezaje kuwafikia watu wenye udongo huu?**

- **Twapaswa kumpenda huyu mtu bila vikwazo na tusi mhukumu kwa maneno yetu dhidi yake**
- **Tuombe apate kushawishika na apate ufahamu**
- **Tuombe Mungu amuondolee mbale vitu vyote vinavyo mzuia na kumuezesha aone ukweli wa hali ya upungufu wa kiroho**
- **Tuendelee kuwa mfano bora kwao kwa mambo ya Mungu na kazi yake**

**Udongo mzuri: watu wengine wako tayari kupokea Injili:**

**Udongo (ms. 8): "Nyingine zikaanguka penye udongo ulio mzuri, zikazaa matunda, zikmea na kukua, na kuzaa, moja thelathini, moja sitini, na moja mia."**

Maelezo kuhusu huu udongo (ms. 20): "Na hawa ndio waliopandwa penye udongo ulio mzuri; ni watu walisikiao lile neno na kulipokea, na kuzaa matunda, mmoja thelathini, mmoja sitini, na mmoja mia."

Udongo wa nne uko mbali na barabara. Umelimwa kikamilifu. Uko na uwezo wa kutengemeza mmea bila kwekwe. Kwa sababu ya hali, iliweza kuzaa mazao maradufu.

Mazoa iliotokana na udongo huu ni wa kufurahisha sana. Yesu hakuwa akiongela kwa mzaha kuhusu mazoa ya juu yam mmea. Historia inatuonyesha kwamba wakati wa karne ya kwanza, kwamba uwiano wa mazao ya nafaka ungekuwa chini ya nane kwa moja. Uwiano ambao Yesu anayoelezea unawezekana kupitia nguvu za Mungu. Uwiano wake ni wa 30 kwa 1, 60 kwa 1, na 100 kwa moja. Mafundisho haya ni kama ule unao patikana katika kitabu cha Yohana 15 alipoongea kuhusu matunda, matunda mengi, na matunda mengi zaidi.
Matunda ya Mungu huonekana wazi, hauta tafuta sana kujua kama ni ya Kikristo. Utaona mkono wa Mungu kwa kila hali.

Tunawezaje kupokea wtu wenye udongo huu?

Shiriki nao Injili kwa dhahiri, na uwasaidie kuelewa jinsi wanaweza tubu dhambi zao na kuweka imani yao yote kwa Yesu Kristo.

## Injili ni Nini?

- Wewe na mimi tuliumbwa tuwe na uhusiano na Mungu (Mwanzo 2-3; Mambo ya Walawi 26:12).
- Dhambi yetu ilitutenga mbali na Uhusiano na Mungu (Isaia 59:2; Warumi 3:23; 6:23).
- **Hakuna** kitu tunaweza kufanya kuleta upatanisho na Mungu tena kwa nguvu zetu (Waefeso 2:1-9).
- **Yesu ali**kufa msalabani akalipa adhabu ya dhambi zetu (Warumi 5:8-10; Waefeso 2:13-16; 1 Yohana 4:10).
- Yesu alifufuka kutoka kwa wafu ili sisi tuwe na uzima (Petero wa Kwanza 1:3).
- Yesu ametupa uzima wa Milele (ameleta upatanisho) kwa wale watakao tubu dhambi zao na kuweka imani yao kwa yesu Kristo (Yohana 3:16; 17:3; Matendo ya Mitume 2:38; Warumi 10:9)

Tunapo jumuisha maelezo haya yote, tunaona kwamba watu wengine hawaelewi Injili, wengine hawafahamu umuhimu wa kumfuata Kristo, wengine wana furahishwa na ulimwengu, wengine wanakubali Injili. Mpanzi wa mbegu atapanda katika kila udongo. Yule anayevuna atafuatilia sana udongo mzuri unao toa mazao.

Mbali na hayo, haimaanishi kutupilia mbali udongo zongine. Ni makumbusho tusilazimishe, kutumia uwongo, au kuwasukumia watu maombi ya toba. Kwa kuelewa hali ya udongo tofauti, tunaweza kuhubiri neno la Mungu kikamilifu kwa watu tofauti na kuyafikia mahitaji yao ya kiroho.

## Je Msingi wa ujumbe wa Injili ni nini?

- **Wewe na Mimi tuliumbwa tuwe na uhusiano na Mungu** (Mwanzo 2-3; Mambo ya Walawi 26:12)**.**
- **Dhambi yetu ilitutenga mbali na Uhusiano na Mungu** (Isaia 59:2; Warumi 3:23; 6:23)**.**
- **Hakuna kitu tunaweza kufanya kuleta upatanisho na Mungu tena kwa nguvu zetu** (Waefeso 2:1-9)**.**
- **Yesu alikufa msalabani akalipa adhabu ya dhambi zetu** (Warumi 5:8-10; Waefeso 2:13-16; 1 Yohana 4:10)**.**
- **Yesu alifufuka kutoka kwa wafu ili sisi tuwe na uzima** (Petero wa Kwanza 1:3)**.**
- **Yesu ametupa uzima wa Milele** (ameleta upatanisho) **kwa wale watakaao tubu dhambi zao na kuweka imani yao kwa yesu Kristo** (Yohana 3:16; 17:3; Matendo ya Mitume 2:38)**.**

Sehemu ya mwisho ya Hii ndio Injili iko na sehemu nne:

Jinsi rahisi ya kuwasilisha injili , Nakala inayoweza chapishwa itakayo kuwezesha kuwa na vijibu (angalia kiambatisho cha nane), Maelezo zaidi ya kuasilisha injili, na ukurasa moja ya maelezo zaidi ya kawasilisha Injili inayoweza kuchapishwa (angalia kiambatisho cha tisa). Lengo kuu ni kuchungua maelezo kuhusu Neno la Mungu, kufahamu kila sehemu ya Injili, na kutumia maelezo haya na fundisho haya unapo wasilisha ama kufundisha Neno la Mungu kwa watu wengine.

Kushiriki Injili kulingana na mfano huu itawezesha mmoja kuwa wakati mzuri na rahisi ya ya kufuatilia maelezo haya baadaye. Injili inafunza sana kuhusu ushirikiano na uhusiano na mafundisho ya kufuatilia baadaye inatilia mkazo sana watu kuwa na uhusiano na ushirikiano wa karibu.

Kurejelea tena na tena katika kushiriki neno la Mungu ukifuata utaratibu hii, itakusaidia kunukuu akilini na hata washiriki wengine kanisani, katika vikundi vya darasa ya Bibilia, wale wanao pitia mafundisho ya Bibilia na hata wale ambao bado hajaokoka. Lengo ni kuondoa kuchnganyikiwa kwa kurejelea ukweli tena na tena. Baada ya muda, watu watajua na kufahamu Injili kwa sababu wameweza kuisikia maelezo haya zaidi ya mara moja.

Ni muhimu kujifunza maelezo haya na kujifahamisha nayo, pamoja na maandiko kando yake. Si lazima uyaweke akilini kila andiko, lakini ni muhimu kuzinukuu katika bibilia yako. Kuwa na nakala ya taratibu ya kuwasilisha Injili kwenye pochi lako, ndani ya Bibilia, na hata kwa simu.

Kwa kujifahamisha na taratibu hii, soma nakala yenye maelezo zaidi kuhusi jinsi ya kushiriki na kufunza Neno la Mungu. Kila maelezo imefuatiliwa na ufafanuzi wake. Ni muhimu ufahamu kila kipengele na kwa nini ni ya maana iwepo hapo kwa sababu ya Injili.

Ikiwa unshiriki katika Injili na unaye shiriki naye hayuko tayari kupokea Kristo ama kuweka imani yake kwa Krsito, umuachie nakala yenye maelezo zaidi inayofunza kwa undani. Umuombe Mungu awaezshe kupitia mafundisho hayo ulio muachia kwa wakati wao. Maelezo zaidi ni ya muhimu kwako na kwa wenye unao walezea injili, na ina anuani ya mtandao ukihitaji maelezo zaidi.

# *Lengo kuu ya Maisha ni Nini?*

Swali hili limeulizwa kwa karne nyingi. Bibilia inatupa jibu sawia.

## LENGO KUU LA MAISHA NI UHUSIANO.

Kutoka kitabu cha Mwanzo hadi Ufunuo, Bibilia imeongela kwa kina ujumbe wa uhusiano. Ujumbe huu unaitwa Injili (ama Habari Njema).

Mtu anapo elewa ujumbe huu na kuupokea zawadi ya Mungu ya Uzima wa Milele, hawapati lengo la maisha tu bali Maisha yenyewe.

"Yesu akamwambia, "mimi ndimi njia, kweli, na Uzima." —Yohana 14:6

### Wewe na mimi tuliumbwa tuwe na uhusiano na Mungu

Mwanzo 2-3 inatuambia kwamba Adamu aliumbwa kwa mfano wa Mungu na akapwewa uwzo wa kuwa na uhusiano pamoja na Mungu. Hadithi hii inaonyesha mawasiliano, utangamano, ushirikiano na uhusiano kati ya Mungu na Adamu.

Mpango wa Mungu wa kuwa na uhusiano haukuishia kwa Adamu. Aliweka agano la uhusiano na wana wa Israeli. "Nami nitakmwenda kati yenu, name nitakuwa Mungu wenu, nanyi mtakuwa watu wamgu." (Mambo ya Walawi 26:12). Yesu naye alisisitiza umuhimu wa uhusiano kwa kuwashauri wanafunzi wake kukaa ndani yake (Yohana 15:1-10), na kwa kuahidi kujidhihirisha kwao wanao mmpenda (Yohana 14:21), kisha kuwaita wanfunzi wake marafiki zake (Yohana 15:15). Kila mstari wa Bibilia uliotajwa unaonyesha mapenzi ya Mungu ya kuwa na uhusiano na Watu wake.

### Dhambi zetu ndizo zilizotutenga mbali na uhusiano huo

"Kwa maana wote wame tenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu" (Warumi 3:23). Dhambi ni uvunjaji sheria za Mungu, na ina mshahara wake. Warumi 6:23 ina tuambia kwamba mshahara wa dhambi ni nini. "Mshahara wa dhambi ni mauti." Mshahara ni kitu unachopata baada ya kufanya kazi. Kulingana na Bibilia, sisi sote tunastahili kufa.

Bibilia inapoongelea kifo, inamaanisha kutengwa na Mungu. Tunapokufa kimwili, roho zetu huiacha miili yetu. Katika hali hiyo hiyo, tunapokufa kiroho kwa sababu ya dhambi zetu, roho zetu zina tengana na na Roho wa Mungu. "Lakini dhambi zenu zimewatenganisha nyinyi na Mungu wenu." (Isaiya 59:2).

### Hakuna kitu tunachoweza kufanya kuleta upatanisho ili kurejesha uhusiano wetu na Mungu

Kuna watu wengi wanao amini kuwa matendo mazuri itawaleta karibu na Mungu. Lakusikitisha ni, hakuna kiwango cha kutosha kinacho weza tosheleza uzuri huo. Bibilia haijatuambia, "Kama wewe ni mwema wakati wote, utakubalika na Mungu." Ama, matendo mazuri itfutilia mbali matendo mabaya. Bila kuwa na kipimo cha kujua uzuri wa kufuatiliwa na kila mtu, je, uzuri wawezaje kuwa wa Kutosha?

Bibilia inatusaidia kuon shida yetu si kukosa kuwa na uzuri au wema; shida yetu ni athari ya dhambi. Hatungeweza kuwa na upatanisho wa uhusiano wetu na Mungu kwa sababu dhambi huleta kifo na udanganyifu. Waefeso 2:1 inatufunza kwamba bila Kristo, tumekufa ndani ya dhambi zetu na maovu. Wakorintho wa Pili 4:3,4 inatuonyesha wazi kwamba bila Mungu kuhusika tumefichwa kuona na kujua ukweli na mungu wa ulimwengu huu. Hatuwezi kufanya chochote cha kuleta upatanisho huu na Mungu kwa sababu watu wafu hawan uhai wa kufanya chochote na watu waliodanganywa hawawezi kuamini chochote.

### Yesu alikufa msalabani kulipa adhabu ya dhambi zetu

Adhabu ya dhambi ilikua ni mauti. Yesu alikufa msalabani kulipa hii adhabu kwa sababu ya dhambi zetu. Dhabihu aliyoitoa ilifanya upatanisho ikawezekana. "Kwa maana ikiwa tulipokuwa adui, tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya mwana wake; zaidi sana baada ya kupatanishwa tutaokolewa katika uzima wake." (Warumi 5:10).

### Yesu alifufuka kutoka kwa wafu ili nasi tuwe na uzima

Kama vile kifo cha Yesu kili lipa adhabu ya dhambi zetu, vilevile kufufuka kwake kulituletea matumaini ya uzima wa milele. "Ahimidiwe Mungu Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa rehema zake nyingi alituzaa mara ya pili ili tupate tumaini lenye uzima kwa kufufuka kwake Yesu Kristo katika wafu,..." (Petero wa kwanza 1:3).

Kifo cha Yesu kililipa deni ya dhambi zetu; kufufuka kwa yesu kilifanya uhusiano wetu na Mungu kuwa wa Kweli.

### Yesu anapeana uzima wa milele kwa wale wote watakao tubu dhambi zao kwa kuweka imani yao kwake

Yesu aliongea kuhusu uzima wa milele (Yohana 3:15, 16; 4:14; 5:39; 6:40). Watu wengi wanachlkulia jambo hili la uzima wa milele kuwa la mzaha kama ni kufa pekee. Sivyo vile yesu alivyosema. Katika Yohana 17:3 Yesu alisema, "Na uzima wa milele ndio huu, wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma." Uzima wa milele ni kumjua Mungu. Ni kuijua na kuishi maisha ya upatanisho wenye uhusiano na Mungu.

Kulingana na Bibilia, uzima wa milele imepewa wale watakao geuka mbali na dhambi zao kwa kuweka imani yao ndani ya Kristo na kazi aliyoifanya kwa sababu yao. Bibilia inaelezea zaidi hali hii ya kugeuka mbali na dhambi kupitia halli ya kukiri nakutubu dhambi. Haimaanishi kwamba mtu atakuwa bila dhambi. Ina maana kwamba wanampenda Mungu zaidi kuliko matendo yao ya dhambi.

## *Nawezaje kupokea uzima wa milele?*

Yohana 3:36 inatuambia, "Amwaminiye Mwana yuna uzima wa milele; asiyemwamini Mwana hataona uzima, bali ghadhabu ya Mungu inamkalia."Mtu anapokea uzima wa milele kwa kuweka imani yake kwa kile Yesu Kristo alicho wafanyia. Yesu aliwafanyia nini? Alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zao, alifufuka kutoka kwa wafu ili nao wapate huo uzima, na amewapa uzima wa milele kwa yeyote atakaye tubu dhambi zake na kuweka imani yake kwake Kristo.

Kumfuata Kristo ni safari isiyokuwa na mnwisho, lakini ina mwanzo ya kupitia maombi itakayo kukuongoza maishani. "Mungu najua kwamba nimetenda dhambi. Nimetambua kwamba dhambi zangu ndizo zimenitenga na wewe. Naamini yesu alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zangu, na alifufuka tena siku ya tatu. Kama vile ninavyo jua vyema, nageuka mbali na dhambi zangu na ninweka imani yangu ndani ya Yesu na kile alicho nitendea mimi. Katika Jina la Yesu nimeomba, Amina."

---

Kama umeweka imani yako kwa Yesu leo, tunakuimiza ushuhudie uamuzi wako kwa wengine. Kwa mafundisho zaidi kuhusu uhusiano wako mpya na Mungu, Nenda kwenye mtandao **www.thisisthegospel.com**.

## *KARIBU KWA FAMILIA HII*

Galatians 4:7